

## KIZUDUO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA UKERWE  
MKOA WA MWANZA**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA CMT KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI  
MDOGO WA MIKUTANO CHA TAREHE 13/1/2022**

### MAHUDHURIO

#### A: WAJUMBE

1. Goodluck J. Mtigandi, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) - Mwenyekiti
2. Boniface Kasema, Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira - Mjumbe
3. Longino Sondole, Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara - Mjumbe
4. Kisesa Katwe, Afisa Biashara - Mjumbe
5. Joseph Komba, Mhasibu Mapato - Mjumbe
6. William Kaswahili, Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika - Mjumbe
7. Hellen N. Rocky, Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii - Mjumbe
8. Abbakary Murshid, Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi - Mjumbe
9. Mhozya Simeo, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi - Mjumbe
10. Deus John, Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi - Mjumbe
11. Paschal B. Malecha, Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili - Mjumbe
12. Joachim Tungilo, Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji - Mjumbe
13. Jenitha Damaseni, Mratibu TASAF - Mjumbe
14. Eng. Hassan H. Shaban, Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi - Mjumbe
15. Majura Kasika, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani - Mjumbe
16. Evarist Msule, Kny Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari - Mjumbe
17. Stephen Kushoka, Katibu TSC - Mjumbe
18. Zaituni Kayanda, Mthibiti Mkuu wa Shule - Mjumbe
19. Dr. Getera Nyangi, Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya - Mjumbe
20. Selemani A. Shabani, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA - Mjumbe
21. Mang'oha Maginga, Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi - Katibu

#### B: SEKRETARIETI

1. Stanford N. Majala - Karani

**MUHT.CMT.NA. 1/2022/1: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe waliohudhuria kikao hicho.

Alifungua kikao saa 2:47 asubuhi.

**MUHT.CMT.NA. 1/2022/2: KUTHIBITISHA AGENDA**

Agenda zifuatazo zilithibitishwa kwenye kikao.

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Taarifa ya utekelezaji wa miradi iliyotekelezwa kwa fedha toka IMF (UVIKO 19) yenye thamani ya Tsh. 3,420,000,000.00
4. Kufunga kikao

**MUHT.CMT.NA. 1/2022/3: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI ILIYOTEKELEZWA KWA FEDHA TOKA IMF (UVIKO 19) YENYE THAMANI YA TSH. 3,420,000,000.**

Taarifa iliwasilishwa kwenye kikao ikioesha kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe tarehe 20 Oktoba, 2021 ilipokea fedha kiasi cha Tsh. 3,420,000,000.00 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali kwenye sekta za elimu, ambapo elimu sekondari ilipokea fedha kiasi cha Tsh. 3,100,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 155 kwenye shule za sekondari 26 na elimu msingi ilipokea fedha kiasi cha Tsh. 240,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 12 kwenye shule za msingi shikizi 3 pamoja na ujenzi wa bweni 1 kwa thamani ya Tsh. 80,000,000.00 kwenye shule ya msingi 1.

Hali ya mradi, ujenzi wa vyumba vya madarasa 155 kwa shule za sekondari na madarasa 12 kwa shule za msingi shikizi umekamilika na yanatumika, ujenzi wa bweni 1 limezekwa na kiasi cha Tsh. 53,374,695.00 kinahitajika ili kukamilisha mradi huo.

Taarifa ilipokelewa na kuridhiwa.

**MUHT.CMT.NA. 1/2022/4: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wote waliohudhuria kikao hicho.

Alifunga kikao saa 5:15 asubuhi.

**UMETHIBITISHWA**

**KATIBU**

**MWENYEKITI**

JINA: Mang'oha Pagiinga

JINA: Goodluck S. Mwandishi

SAINI: Elyda

SAINI: Jh

TAREHE: 13 / 1 / 2022

TAREHE: 13 / 1 / 2022